**102/2**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA SPEC PRE-MOCK 2026**

---

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

(a) Ni mfumo wa mawasiliano katika jamii yoyote ile. (alama 2)

(b) Lugha ya taifa na ile inayoteuliwa kutumia katika shughuli zote za taifa ambayo hueneza umoja na uelewano katika jamii ilhali lugha ya kikazi ni ile inayotumiwa kuendesha shughuli rasmi za taifa. (alama 2)

(c) (i) Huhitajika ili kueneza maongozi ya taifa ya kuleta ufahamikiano kote nchini.
(ii) Ili kuvunja na kukomesha hisia za kibinafsi na kikabila. (alama 2)

(d) (i) Ni chombo cha mawasiliano katika nyanja za elimu, biashara, maandishi na siasa.
(ii) Ni kiungo cha kueneza umoja na maelewano miongoni mwa jamii tofauti.
(iii) Ni kitambulisho cha utaifa. (alama 3)

(e) (i) Haiwezekani.
(ii) Matendo na hulka za binadamu.
(iii) Mfano
(iv) Mazingira (alama 4)

(f) (i) Ni chombo cha mawasiliano.
(ii) Ni kielelezo cha fikra na hisia za binadamu. (alama 2)

## 2. MAJIBU YA MUHTASARI

(a)
(i) Binadamu huishi kwa kutangamana.
(ii) Binadamu huathiriana kitabia, kifikiria, kimavazi na kimaisha.
(iii) Watu wote wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa.
(iv) Wanaoathiriwa zaidi ni mahirimu wao na vijana.

(v) Hali ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika.
(vi) Wattu wazima pia huathiriwa na wenzao.
(vii) Watu wote wanaweza kuathiriwa na shinikizo-rika,.
(viii) Ni vigumu kukabiliana na shinikizo-rika. (alama 7, 1 ya utiririko)

(b)
(i) Shinikizo-rika hujitokeza kwa sura nyingi.
(ii) Kulazimisha watu kutenda kinyume na imani yao.
(iii) Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kugengwa na wenzao.
(iv) Pia wanaweza kutishwa kwa kutumia mabavu.
(v) Wanaoshinikizwa wasimame kidete na watetee msimamo wao.
(vi) Wanasaikolojia wanapendekeza watu wajiamini.
(vii) Asiyejiamini atahangaishwa na wenzake. (alama 6, 1 ya utiriko)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

(a) (i) / e /

*1.* Mbele
*2.* Kati
*3.* Mtandazo

(ii) / u /

1. nyuma
2. juu
3. mviringo

(b) Nyakua – KI / KKI – 1 x 1

Chura – KI ala 1 x 1

(c) Wachache walifika jioni. (1 x 2 = 2) (Kadiria kiwakilishi jumla)

(d)

| S | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KN | | | | KT | | | |
| N | V | E | S | T | H | N | V |
| mkongojo | mrefu | sana | ulioletewa babu | utauzwa | na | fundi | mcheshi |

(12 x 1/3 = 4)

(e) Mtoto msichana amemeza dawa. (1x2 = 2)

(f) Nisipompiku masomoni sitatuzwa zawadi. (1x2)

(g) "Watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu," chifu wetu alituambia.

(6 x ½ = 3)

Au Chifu wetu alituambia, "Watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu."

(h) (i) –La – Lishia (ala 1x1 =1)

(ii) toa – toleka (ala 1x1 = 1)

(i) Matumizi ya alama ya mshangao (!)

1. Kushangaa
2. Kuamrisha (ala 1x1 = 1)

Kiulizi

(i) Kuuliza swali (1 x 1 = 1)

(j) A

LI – wakati uliopita

vyo

li – mtendwa

kimbi

li – kauli

(k) Mwanafunzi alimwandikia rafikiye barua kwa penseli.
Kipozi – barua
Ala – penseli (alama 3 x1 = 3)
Kitendo – rafikiye (kadiria sentensi)
(Tanbihi: Mwanfunzi atuzwe alama kwa maneno aliyoyaelekeza.

(l) Mhamiaji haramu aliyeshikwa amefikishwa mahakamani.
a – kishazi tegemezi
b – kishazi huru

(m) Wingi karibu
Watu wawa hawa waliibeba mizigo ii hii licha ya kukanywa. (alama 1 x 2)

(n) Mbunge atakuwa ametawazwa kabla ya mpinzani wake kufika. (alama 1x2 =2)

(o) Ngoma hii itachezwa wanjani. (alama 1x1)

*Mwanafunzi asiandike wastana wa kielezi.*

(p) Matumizi ya kiimbo
- Swali
- Rai / ombi — Kutaja (2 x 1 = 2)
- Amri
- Mshangao — Kutunga sentensi (2 x 1 = 2)
- Taarifa

(q) Mbuzi – Kifaa cha kukunia nazi.
- Mnyama

**ISIMU JAMII**

4. (a)
– Lugha yenye ukali kw. Polisi.
– Lugha ya kudhadisi/maswali ni majibu.
– Kuchanganya ndimi.
– Lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi.
– Lugha ya unyenyekevu kwa mshukiwa.
– Lugha ya kuamrisha.
– Lugha inayoeleweka kwa urahisi
– Lugha ya misimu.

(5 x 1 = 5)

(b) Eleza maana ya istillahi zifuatazo za isimu jamii.
– Lugha ya taifa – Ni lugha iliyotenliwa kama kitambulisho na ustaarabu wa taifa zima.
– Lugha ishara – Ni lugha inayotumia ishara kama mikono, uso ni macho katika kuwasiliana.
– Lugha mwiko – Lugha inayomfunga mtu kuitumia kwa mujibu wa jamii yake.
– Sajili za lugha – Mitindo mbalimbali ya matumizi ya ile lugha moja.
– Uchanganyaji msimbo – Ni hali ambapo wazungumzaji wa lugha wanazungumza katika
– lugha moja kisha hapa na pale wanatoka kidogo katika lugha hiyo na kuingilia lugha ya pili au ya tatu kwa muda mfupi na kisha kurejelea lugha ya awali.